

# UQAB
Jarida la

*Toleo 24 - Rabi-ul-Thani 1440 H / Januari 2019 Miladi*


**Siku ya Jamhuri: Miaka 55 ya Uhuru Bandia!**


**Juhudi za Uturuki Zitafaulu?**

**Vita dhidi ya Ufisadi**

**Nidhamu za Mahakama Zilizodorora**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 19**

**SWALI/JAWABU: Utawala wa Dola Juu ya Uchumi wa Kiulimwengu**

## “Na nani aliye mbora zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu”

uqab.or.ke    uqab_htk    UQAB-Magazine-1911964012162253

KUMB: 07/1440 | Ijumaa, 29 Rabi ul Awal 1440 H | 07/12/2018 M

# Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Tunisia Inatangaza Uzinduzi wa Kampeni

# (وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللهِ حُكْماً...)

# "Na nani aliye mbora zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu"

# (Imetafsiriwa)

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Tunisia hivi sasa imo katika kipindi kigumu baada ya wale tuliowafikiria kuwa ni watawala kuyatelekeza majukumu yao msingi na kuziwachia dola za msalaba za kikoloni na wafanyikazi wake ndani ya Umoja wa Ulaya na Shirika la Fedha la Kimataifa kuamua sera za kiuchumi, kifedha na kijamii mpaka nchi ikadhibiti usambaratikaji wa kiuchumi licha ya kwamba kulikuwa na madeni makubwa.

Kutokana na ushindani wa kisiasa nchini na kushughulishwa kwa vyama tawala kutokana na mizozo yao ya kindani badala ya kulifanyiakazi taifa. Na upande mwingine watu wamekata tamaa na nidhamu ya kisiasa na vyama vya udanganyifu, ambayo ilidhihirishwa kwa kuepuka upigaji kura za Manispaa zilizopita. Sisi katika Hizb ut Tahrir/ Wilayah ya Tunisia tunatangaza kwa Ummah uzinduzi wa kampeni ya kisiasa ili kutoa muongozo kwa wale wanaofikiria kisiasa ili kuwapelekea kutoa suluhisho msingi juu ya matatizo ya Ummah na kuukomboa kutokana na aina zote za ukoloni na utumwa, kwa kusimamisha nidhamu ya kisiasa ya kiutawala, kiuchumi na kijamii kwa msingi wa Uislamu na vipengee vyake vya kisheria.

Kampeni hii mpya, ambayo tumeichagulia kichwa:(وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللهِ حُكْماً) "Na nani aliye mbora zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu" itaendelea kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kwa wiki kadhaa na itakuwa ni fursa ya kuonyesha uwezo wa nidhamu ya Kiislamu katika kuleta mabadiliko msingi ambayo Bwana wa Ulimwengu ametutaka sisi tujikombowe kutokana na madhalimu, vibaraka wakoloni na tuishi kwa hadhi na izza ndani ya nidhamu ambayo inahifahdi itikadi na ustaarabu wa Ummah na kudhamini haki ya kumchagua nani wa kutawala.

Enyi Waislamu ndani ya nchi ya Zaytouna:

Sisi katika Hizb ut Tahrir/Wilayah ya Tunisia tunawaalika mushirikiane nasi katika kampeni hii, na muweke wazi hisia zenu katika kuzikataa sera za kikoloni ambazo zinalenga kuitia katika utumwa nchi hii na watu wake, na mufanyekazi kwa bidii pamoja na mukhlisina na watu wa nguvu ili waweze kuinusuru Dini yao, watu wao na Ummah kwa lengo la kuingia katika historia na cheo kikubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kutokana na kuwaridhia kwake.

(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ)

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." [Al-Anfaal: 24].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah ya Tunisia**

# Siku ya Jamhuri: Miaka 55 ya Uhuru Bandia!





Kenya tarehe 12 Disemba 2018 ili sherehekea Siku ya Jamhuri ili kuadhimisha Miaka 55 tangu kupata “Uhuru Bandia” tarehe 1 Juni 1963. Ukweli ni kwamba Ufalme wa Uingereza ulibadilisha tu wasimamizi wa shamba “koloni” lake Kenya kutoka kwa Gavana Malcolm Macdonald- mzungu hadi kwa Rais Jomo Kenyatta – muafrika. Raisi Jomo Kenyatta alikabidhiwa nyenzo za mamlaka na Prince Philip, mumewe Malikia Elizabeth II. Malcolm Macdonald alirudi tena Kenya na kuwa Kamishna Mkuu wa Uingereza wa kwanza. Na alipokufa Jomo Kenyatta –Prince Charles mtoto wa Malikia Elizabeth II alikuweko mazishini kama asante kwa kazi nzuri! Kila kitu ikiwemo sera na mipango inayotumika kuendesha shamba la mkoloni “Kenya” zimebakia zile zile hadi leo isipokuwa tofauti ni rangi za wasimamizi tu kutoka kwa wazungu hadi waafrika. Ili tufahamu hilo tutataja mifano baadhi tu kama ifuatavyo:

**Kwanza:** Kenya inatawaliwa na mfumo wa kisekula wa kirasilimali uliorithiwa kutoka kwa wakoloni waliotutawala na wanaendelea hadi sasa kupitia vibaraka wao. Mfumo huu umekitwa juu ya ufisadi mkubwa nao ni kumtenga Muumba katika maisha na badala yake kumwachia mwanadamu kujiendeshea mambo anavyotaka kwa kichwa chake ambacho hakidiriki dhati ya Muumba katika kuwapangilia maisha ya viumbe wake. Kipimo chake kikiwa ni maslahi pekee.

**Pili:** Kupitia utekelezwaji wa mfumo huu batili na nidhamu zake zinatokamana nao imepelekea kukithiri kwa ufisadi kila nyanja ikiwemo nidhamu yake ya kisiasa; ambayo inafahamika kama demokrasia. Inampa mwanadamu fursa kumpa mamlaka mwanadamu mwenziwe akamuwakilishe katika utungwaji wa sheria ili ziwaongoze katika maisha jumla. Siasa hizi zimepelekea kukithirisha ukabila kwa kuwa daima wakoloni wameifunga siasa juu ya kabila kubwa na zenye nguvu. Kiasi kwamba siasa imekuwa ni kinyang’anyiro kati ya makabila!


**Tatu:** Nidhamu ya uchumi ambao unaendeshwa kwa njia ya uporaji ambao ulianza tokea ukoloni wa moja kwa moja hadi wa leo. Mali za taifa zimetekwa na kuwa za wakoloni na vibaraka wao, ikiwemo ardhi, mabiashara msingi n.k. Raia jumla wamebakia kudidimizwa katika umasikini wa kupindukia kila kukicha kupitia kutozwa kodi zisizokuwa na huruma na ukopaji wa mikopo ya riba isiyoingia akilini. Huku kashfa za ufujaji wa mabilioni ya fedha ukiendelea daima!

**Nne:** Nidhamu ya kijamii imekitwa juu ya uhuru; kiasi kwamba ubinafsi umekithiri na kila mmoja yuwenda mbio ili kujistarehesha kwa kiwango cha juu kwa njia yoyote wakati wowote ule. Madhara yake katika jamii yakiwa ni yakushtusha na kuvunja moyo na kukatisha tamaa wengi wa watu na kuwapelekea watu kuwa kama wanyama au chini zaid kwa kutenda vitendo baadhi ya mfano kuvunja familia, uzinifu, usagaji, ushoga, , ulafi wa mali, kujiua, n.k! Hii ikiwa imechangiwa pakubwa na nidhamu ya kielimu ambayo inajenga kuzalisha vikaragosi kwa sura za watu lakini wenye mitizamo ya kiyahayawani iliyofungwa tu katika kipimo cha faida na hasara. Na kuipelekea thamani ya mtu kutegemea kitu/ mali aliyokuwa nayo/anayozalisha.

Suluhisho na Uhuru wa kweli ni ule utakaohakikisha kuwa Kenya inatawaliwa na mfumo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kujua kizuri na kibaya kwa viumbe wake. Mfumo unaotoka kwa Mola ni ule wa Uislamu na unatakiwa kutekelezwa na Dola ya Kiislamu ya Khilafah iliyosimama kwa njia ya Utume. Kupitia kusimamishwa kwa Khilafah ndiko kutakakopelekea si tu Kenya bali Afrika kukombolewa kutoka katika utumwa wa kikoloni, vibaraka wake na mfumo wao muovu na nidhamu zake ambao ndio chanzo cha kusambaratika Kenya, Afrika na Ulimwengu kwa ujumla.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Juhudi za Uturuki Kuichafua Saudi Arabia Mbele ya Wamagharibi Zitafaulu?




Tokea tarehe 02/10/2018 ulimwengu umeshuhudia juhudi na kampeni za kila aina za serikali ya Uturuki ili kuondoa haiba ya serikali ya Saudi Arabia pamoja na mrithi wa kiti cha kifalme Mohammed bin Salman kwa mauaji ya kinyama aliyofanyiwa Jamal Khashoggi ndani ya ubalozi wa Saudia huko Instanbul.

Juhudi zilizochukuliwa na Instanbul ni ile ya mwanasheria wa serikali ya Uturuki kutoa waranti ya kukamatwa kwa wasaidizi wa Mohammed bin Salman: Saud al-Qahtani na Jenerali Ahmed Asiri, ambao tayari Riyadh imewauzulu nafasi zao. Juhudi nyengine ni kuachia rekodi za mauaji hayo kwa Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Saudia. Hii ni kwa mujibu wa vyombo vya habari vilivyomnukuu Rais Erdogan kabla kwenda Ufaransa katika sherehe za Kusitishwa kwa Vita (Armistice).

Ingawa Wamagharibi na taasisi zao wameitikia na kufanyia kazi juhudi za Uturuki kama vile CIA chini ya Mkurugenzi wake Gina Haspel alivyoweka wazi mbele ya Seneti kuhusu ushahidi unaoonesha kuwa Muhammad bin Salman kuhusika na Kiongozi Mkuu wa Seneti wa Republican Lindsey Graham kwa kusema kuwa hamna shaka (zero chance) kuwa Mohammed bin Salman anahusika. Pia Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, Michelle Bachelet ametaka ufanyike uchunguzi wa kimataifa juu ya kadhia hiyo.

Juhudi zote hizi za Uturuki si kama wanampenda Khashoggi au wana ubinadamu kwani serikali hiyo kama zilivyo nyengine zinanuka damu ya mamia ya watu wasio na hatia kwani chini ya Erdogan, ulimwengu umeshuhudia mamia ya Waturuki wakitiwa kizuizini, kuteswa na propaganda nyingi dhidi ya wapinzani wake wakiwemo wasomi, waandishi wa habari, masheikh, wanaharakati, wanajeshi na wanachama wa Hizb ut Tahrir hasa baada ya mapinduzi bandia (proxy coup).

Rais Trump amesema wazi hatositisha mpango wa serikali ya Marekani wa kuiuzia serikali ya Saudi Arabia silaha za mamilioni ya dola. Pia alipokuwa Buenos Aires Mohammed bin Salman aliweza kubadilishana mawazo na Rais wa Urusi, Vladmir Putin kwa furaha.

Kwa viashiria hivi na vyenginevyo, harakati za Istanbul zenye lengo la kuutikisa na kuushughulisha utawala wa Riyadh, na lengo kubwa zaidi ni kutaka kuipata hadhi na nafasi ya Saudia mbele ya Wamagharibi jambo ambalo si rahisi kwa Uturuki kulifikia na haitalifikia kamwe pamoja na yote yaliyotokea.

Saudia itabakia ni mboni ya jicho kwa Wamagharibi kuliko Uturuki kama vile zilivyo umbile la Kiyahudi (Israel) na Misri. Sababu zinazoifanya Saudia iwe na umuhimu kwa Wamagharibi ni nyingi na ndio maana Afisa wa ngazi ya juu ya utawala wa Trump alisema “hali ni tete kwa tukio la mauaji ya Khashoggi na ni changamoto ya hali ya juu kwa sera ya kigeni ya Marekani wanayo kabiliana nayo.”

Mambo yanayoifanya Saudia iwe na nafasi ya pekee kwa Wamagharibi ni kama zifuatazo:

- Kwanza muundo wa siasa za ndani za Uturuki ni rahisi zaidi kubadilisha sura ya vibaraka kuliko Saudia, kwani

*Endelea Uk..5*


Email: info@uqab.or.ke

hakuna mbadala wa ukoo wala harakati ambayo itakuwa ni rahisi kwa Wamagharibi kubadilisha mbali na ukoo wa bin Saud, hivyo ina walazimu wakubaliane na ukoo huo japo wanaweza kumbadilisha mrithi wa ufalme kama walivyo badilishwa wengi huko nyuma au hata hivi karibuni alivyobadilishwa na kupewa nafasi Mohammed bin Salman.

- Nafasi ya Saudia katika ulimwengu wa Waislamu hasa Wakisunni ambapo Waislamu wengi wanauona utawala wa Kisaudi ni wao, hivyo kuwaunga mkono ni kama wajib kwao tofauti na Uturuki ambayo Waislamu wengi wanawaona kama wazungu na Wamagharibi yaani hawana ushawishi mbele ya Ummah wa Waislamu.
- Utawala wa Riyadh unawasaidia sana Wamagharibi katika kuharibu sura ya Uislamu kwa kutoa wasomi wa dini ambao husambazwa dunia nzima kupeleka ufahamu huo wa kimakosa, ingawa Uturuki inafanya hayo hayo lakini Saudia haizidiwi na dola yoyote duniani kwanza kwa historia yake ya Uislamu.
- Nafasi ya Saudia katika kuvuruga umoja wa Waislamu duniani hailingani na ya Uturuki, hivyo Wamagharibi ni lazima waung'ang'anie utawala wa Riyadh ili kutimiza lengo hili kwa kusaidiwa na Iran kwa upande wa pili kwa kupandisha hamasa za kimadhehbu kati ya Sunni na Shia.
- Ukiachilia Misri ambayo inalilindi umbile la Kiyahudi (Israel), hakuna nchi ambayo ina nafasi kubwa katika kulihifadhi umbile la Kiyahudi (Israel) zaidi ya Saudi Arabia. Kwani viongozi wake wamekuwa watiifu na kuweza kuwasaidia Mayahudi nyuma ya pazia ilhali wanapaza sauti za kisanii ili kuwadanganya Waislamu ili waonekane kuwa wao ni mashujaa.
- Saudia imejikabidhi kwa Wamagharibi kwa kila kitu kana kwamba ni jimbo moja la Wamagharibi. Hivyo inalindwa na kukabidhisha kambi na miradi yake yote kwa Wamagharibi, ingawa Instanbul inafanya kama Saudia lakini Saudia imezidi na ndio Trump aliwaambia tukiacha kuwalinda sisi munaanguka.
- Katika Mashariki ya Kati, Saudia imekuwa na ushawishi mkubwa sana kwa baadhi ya nchi kama vile Falme za Kiarabu, Kuwait, Sudan, Tunisia, Morocco, Jordan na nchi zilizobakia kama Lebanon, Yemen, Syria na Iraq imekuwa ina mlingano sawa na Iran nafasi ambayo Uturuki haina.
- Upande wa kiuchumi Saudia ina umuhimu mkubwa kutokana na uwezo wake mkubwa wa visima vya mafuta. Pia inategemea kila kitu kutoka kwa Wamagharibi hata kwa kitu kama tishu tafauti na Uturuki ambayo ina vijiwanda kadhaa.

Kwa hivyo kadiri ya Uturuki inavyofanya kuushawishi ulimwengu wa Kimagharibi ili kuondoa nafasi ya Saudia haitafaulu, kwa kuwa Saudia ina nafasi kubwa kwa maslahi ya Wamagharibi ya kuuhujumu Uislamu na pia malengo ya kimali kuliko Uturuki.

**Ali Amour**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

HIZB UT TAHRIR

KUMB: 02/1440 | Ijumatatu, 03 Rabi ul Thani 1440 H | 10/12/2018 M


# Vita dhidi ya Ufisadi kattu havitoshinda chini ya Mfumo fisidifu wa Kirasilimali

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Muhula wa pili wa rais Uhuru Kenyatta umekumbwa na msururu wa kashfa za ufisadi kwenye idara mbalimbali za Serikali. Kashfa tano tayari zimefichuka ndani ya mashirika makubwa ya umma jambo linaloonesha kuzagaa kwa jinamizi hili la ufisadi. Kashfa ya hivi karibuni ikiwa ni ile inayokumba shirika la usambazaji wa mafuta nchini (KPC) ambapo lita za mafuta milioni 11 zimepotea. Huku kampeni ya Uhuru ya kupambana na ufisadi ikionekana kuteka hisia kubwa za raia, sisi **Hizb ut Tahrir /Kenya** tungependa kusema yafuatayo:-

**Kwanza:** Ni udhalimu mkubwa ma-afisa wa ngazi za juu serikalini waliobebeshwa jukumu la kusimamia maslahi ya umma kuwaona wakishindana katika kufuja rasilimali za umma badala ya wao kuboresha maisha ya wananchi wa kawaida.

**Pili:** Kamatakamata ya wakuu wa mashirika kadhaa inayoshuhudiwa kwa sasa si lolote ila sarakasi ya kisiasa tu inayolenga kuhadaa kina yakhe waamini kuwa vita dhidi ya ufisadi ni vyenye kushinda ndani ya mfumo wa kirasilimali. Na hilo halina ukweli hata chembe kwani washukiwa wengi wa ufisadi walioshtakiwa mahakamani hivi karibuni wamekuwa wakionekana wakiachwa huru kwa madai ya 'kukosekana ushahidi'. Fauka ya hilo linalopaswa kueleweka ni kuwa Kenya imejifunga na mfumo wa Kibepari uliopandikiza tamaa ya fisi ya kutaka kujilimbikizia mali kwa njia na mbinu zote chafu uhalisia unaofanya kuwa vita dhidi ya ufisadi kamwe havitofua dafu. Mfumo huu muovu umefanya maslahi kuwa ndio kipimo pekee cha kupeleka maisha ya wanadamu jambo linalowafanya watu hasa walioko serikalini kupatiliza fursa ya kung'anga'nia mali kwa mbinu chafu.

**Tatu:** Ufisadi wa ma-afisa wa kiserikali utawezwa kuondoshwa tu chini ya Uislamu kupitia utawala wake wa Khilafah ambapo kiongozi (Khalifah) hutekeleza sheria za Mwenyezi Mungu (swt). Sheria ambazo huonesha njia ya serikali ya ukusanyaji na matumizi ya rasilimali zake. Isitoshe, Uislamu umewajibisha kuwa afisa yeyote lazima achunguzwe kimakini kabla hajaingia afisini na hata akiondoka. Hili ni kuwa mapato yoyote atakayoyapata mfanyikazi wa serikali kinyume na utaratibu wa kazi yake yatataifishwa na kurudishwa kwa hazina ya serikali (Baitul Mal). Kwa haya tunasema kwamba Khilafah pekee kwa Mfumo wa bwana Mtume (saw) ndio itakomesha tatizo la ufisadi sio tu kwa Kenya bali ulimwengu mzima.


**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# Nidhamu za Mahakama Zilizodorora Ndani ya Ardhi za Waislamu Zina Wafelisha Wanawake na Familia

Ummah wa Waislamu ni mmoja, lakini kivitendo tumegawanyika zaidi ya mataifa 50. Kila dola ina katiba yake na utekelezwaji wa Uislamu safi unatofautiana katika kila nyanja kuanzia kubwa hadi ndogo. Dola nyingi za Waislamu zinadanganya kuwa zinatekeleza Uislamu lakini zinatekeleza sheria zinazotokamana na akili za wanadamu. Kwani hivi sasa muundo wa serikali unafanyakazi ndani ya vitengo vya bunge, baraza la mawaziri na mahakama. Sheria zinazotungwa, zinazotekelezwa na kulindwa na taasisi hizi tatu ndiyo msingi wa maisha ya raia wanaoishi ndani ya dola. Jukumu la wanachama wa taasisi hizi ni kutunga, kutekeleza na kulinda sheria ambazo lengo lake ni kusuluhisha matatizo ambayo wanadamu wanakabiliana nayo kila siku. Lakusikitisha, taasisi hizi zenyewe zinaweza kuwa ni sehemu ya tatizo na huu ndiyo uhalisia tunaouona ndani ya ulimwengu wa Waislamu leo.

Hususan wanawake wanakabiliana na hali ambayo maisha yao yamejaa matatizo ambayo hayatatuliwi. Kila siku, wanawake wengi Waislamu wanakabiliana na matatizo ya ndoa za lazima. Pindi wanapoolewa, wanakabiliana na matatizo yanayohusiana na dhuluma za kinyumbani. Na wanapotaka kuvunjwa kwa ndoa, huwa ni mchakato mgumu. Wanawake wanaofaulu kupewa talaka au khula mara nyingi hukumbana na matatizo ya kurudisha haki yao ya mahari na mali za kibinafsi, au matatizo ya ulezi wa mtoto na uhifadhi. Matukio haya yakuvunja moyo yanaripotiwa kila siku katika magazeti ya kitaifa. Sababu za matatizo haya zinakinzana. Mashirika ya haki za binadamu wanalaumu maadili ya kidini na tamaduni. Lakini pindi matatizo yanapotokea, wanawake ambao hawawezi kuyatatua kupitia familia wanazielekea nidhamu za mahakama za dola.  Nidhamu za mahakama ndani ya nchi za Waislamu ambazo zimekitwa juu ya sheria za kisekula, hazihakikishi kuwa matatizo ya wanawake yametatuliwa kwa urahisi. Sheria na serikali zinatenda kazi kizembe kiasi kwamba wanawake wanapata shida kupata haki ya kusuluhishiwa matatizo yao.

Mnamo 2011, Express Tribune ilitoa ripoti kuhusu mwanamke wa Pakistan, Mai ambaye alishambuliwa na kuvunjiwa heshimiwa baada ya kaka yake mdogo aliposhtumiwa kuwa na mahusiano na mwanamke kutoka katika familia yenye mamlaka kijijini. Aliwapeleka wanaume hao mahakamani lakini 1 pekee alihukumiwa ilhali wengine waliachiliwa na Mahakama ya Chini. Mai alikata rufaa Mahakama Kuu na iliwachukua miaka 5 kumpatia uamuzi ambao ulikuwa sawa na Mahakama ya Chini.

Mfano wa uzembe wa mahakama na kuchukua muda mrefu katika kesi sio suala la kipekee wala sio tatizo la kipekee la mahakama katika nidhamu zilizopo. Kigezo chengine ni gharama za juu ambazo mtu wa kawaida hazimudu. Kwa mujibu wa ripoti hiyo hiyo, familia iliyotafuta haki baada ya mtoto wao wa kike wa miaka sita aliyevunjiwa heshima iliwabidi kutumia Rupee 150,000 licha ya kuwa wanapokea msaada kutoka kwa Shirika lisilokuwa la Serikali la 'Vita dhidi ya Ubakaji.' Babake mtoto alikuwa anapokea Rupee 3,000 kwa wiki.

Nidhamu ya haki ndani ya Ulimwengu wa Waislamu iko polepole, ya kizembe na gharama mno. Kwa mujibu wa takwimu zilizojumuishwa na Tume ya Sheria na Haki ya Pakistan, kulikuwa na jumla kesi 1,954,868 mahakamani ambazo hazijatolewa uamuzi ndani ya nchi mwishoni mwa 2016. Kuchelewa kwa kesi mahakamani ni kufeli kwa dola kwa kuwa kuharakishwa kupatikana kwa haki ni haki msingi ya kila raia chini ya Kipengee 9 na jukumu msingi la serikali chini Kipengee 37 (d) cha Katiba. Kwa mujibu wa ripoti ya Express Tribune, kesi mahakamani zinaweza kuchukua miongo kadhaa na gharama zake ziko juu kupita hata madai ya mlalamishi.

Uzembe wa nidhamu ya mahakama inaweza kuelezewa kwa idadi kubwa ya kesi ambazo zahitaji kushughulikiwa. Hivi sasa, Dawn News inaripoti kuwa zaidi ya kesi milioni 1.8 hazijashughulikiwa ndani ya mahakama za Pakistan. Hii ni kwa sababu ya matatizo mengi ambayo nidhamu ya kisekula inayazalisha. Jamii imejawa na tamaduni kinyume na Uislamu ambazo zinazalisha matatizo tofauti tofauti yakihusiana na mahusiano ya nje ya ndoa, vurugu, mizozo juu ya matarajio ya kifedha ndani ya ndoa na huku mume na mke na wanafamilia wengine kutotimiza majukumu yao juu ya wengine. Kule kujaa kwa kesi mahakamani ndani ya ardhi za Waislamu ni natija ya muundo mbovu wa nidhamu ya mahakama katika dola hizi ambazo zimebuniwa juu ya mtizamo wa Kimagharibi, ambao umeweka ngazi kadhaa ndani ya nidhamu ya mahakama – mfano mahakama ya kukata rufaa, mahakama ya juu na nyinginezo – ambazo huchelewesha utekelezwaji wa kesi. Hili husababisha kesi kuchukua miaka ili kusuluhishwa.  Napia ni kutokana na serikali za kisekula na zisizokuwa za Kiislamu ndani ya ardhi zetu ambazo hazijali uhakikishaji wa kupatikana kwa haki na kusuluhisha matatizo ya watu kiukweli bali wanajali tu kuhifadhi viti vyao vya mamlaka. Hivyo basi, hawawekezi vilivyo kuwepo kwa mahakama za kutosha, mahakimu na vigezo vya kisheria kwa watu.

Zaidi ya hayo, nidhamu za mahakama ndani ya ardhi za Waislamu hazifanyi kazi kama mkono wa dola kulinda umoja wa familia na muundo wa familia kama ilivyokuwa chini ya utawala wa Kiislamu uliotangulia. Mahakama hazishughulikii kwa ukamilifu kesi za ndoa za lazima, hali ambazo mahari haikutolewa au mizozo ya kifamilia. Hivi sasa mahakama sio njia ya utatuzi wa mizozo ya ndoa ili kuiunganisha ndoa pamoja, au vurugu za kinyumbani

Endelea Uk..8

ili kumlinda mwanamke, au kuhakikisha mwanamume anaisimamia familia yake vyema, au kuhakikisha kuwa mume na mke wanatekeleza majukumu yao kila mmoja kwa mwenziwe. Zaidi ya hayo kesi za talaka au kesi kuhusu malezi ya watoto huchukua muda mrefu ili kutatua. Hivyo basi, mwanamume, mwanamke na watoto huachwa njia panda wasiweze kuendelea na maisha yao. Huku kukiwa na mzigo mkubwa wa kifedha, watu binafsi wanalazimishwa kuishi ndani ya ndoa za huzuni na dhuluma kwa muda mrefu. Ukiongezea ukosefu wa haki na mahangaiko juu ya kigezo kuwa mamlaka na fedha mara nyingi huathiri matokeo ya kesi mahakamani ndani ya nchi zetu.

Matatizo haya yanakumbana na watu duniani kote ndani ya nchi nyingi, lakini tukitilia maanani nchi za Waislamu tunapata kuwa kuna mtizamo mfulani wa tatizo. Vyanzo vya sheria ambazo ni katiba humaanisha kuwa nchi ikiwa msingi wa siasa yake ni nidhamu ya kisekula ya kidemokrasia, basi pia nidhamu yake ya mahakama itakuwa hivyo. Tofauti kati ya Pakistan na dola nyingine ipo katika sheria ya kikatiba na sio katika dori ya mahakama. Nchi za Waislamu kama Pakistan, hudai kuwa zimejifunga na hukumu za Shariah. Lakini ukweli ni kwamba katiba zao na hivyo mahakama zao zimekitwa juu ya hukumu za kisekula. Hii ikimaanisha kuwa matatizo wanayokumbana nayo wanawake sio kwa sababu ya sheria za Kiislamu na wala sio suluhisho zinazotolewa au hukumu zinazotolewa na mahakama ambazo zinafeli kutatua masuala ambayo familia na wanawake wanakumbana nayo. Ni kutokana na kuwa sheria ambazo zimepeanwa na Muumba ili kulinda na kusuluhisha matatizo ya familia hazipo ndani ya nchi yoyote ya Waislamu leo.

Mnamo Machi 2016, Muhammad Khan Sherani, mwenyekiti wa Baraza la Mfumo wa Kiislamu Pakistan, alisema kuwa haki za wanawake zimelindwa vyema ndani ya sheria za Kiislamu (CBSnews) na yuko sawa kabisa. Sheria ya Kiislamu inawalinda wanawake, haki zao na familia zao. Tatizo ni kuwa sheria ya Kiislamu katika usafi wake haitekelezwi ndani ya ulimwengu wa Waislamu hivi leo. Labda ushahidi kamili wa hili upo katika kauli iliyotolewa na Shaikh Saleh Bin Humaid, mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mahakama nchini Saudi. Alisema kuwa “Tutachukua bora kutoka kwa nidhamu za mahakama ulimwenguni kote.” Lau Uislamu utakuwa ndiyo msingi wa maamuzi na lau Waislamu, tutakuwa na imani kwa Mwenyezi Mungu na kujua bila shaka kwamba Neno Lake ni Sheria kuu, inakuwaje tena tuseme tutachukua ‘bora’ kutoka kwa nidhamu za mahakama? Kwa nini sisi kama Waislamu tuangalie vyanzo vingine kwa ajili ya sheria zetu na ilhali tunayo sheria pana na nidhamu ambazo twaweza kutatulia matatizo yetu na kuhakikisha kwamba haki za kila mmoja ikijumuisha wanawake na watoto zinatekelezwa?

Kauli zilizotolewa na wawakilishi wa serikali ndani ya ulimwengu wa Waislamu zinaonyesha kwamba matatizo yanatokana na mahakama kutokuwa chini ya msingi wa Uislamu na hivyo basi kutotekeleza sheria za Kiislamu. Sheria zinadaiwa kuwa chini ya msingi au kuathiriwa na Shariah lakini si ukweli. Katika nchi za Waislamu, watawala wanatofautisha kati ya sheria za Kiislamu na katiba ya nchi, wakiweka wazi tofauti kati ya hizo mbili, ambayo haitakiwi kuwepo. Huku kutenganishwa kati ya Uislamu na nidhamu ya kutungwa inaonyesha kuwa Uislamu sio chanzo pekee katika kutoa hukumu za mahakama.

Kipengee 227 cha katiba ya Pakistan kinasema kuwa sheria zote zilizopo “zitaletwa pamoja ili ziwiiane na maamrisho ya Uislamu kama ilivyo kwenye Quran na Sunnah […] na hakuna sheria itakayopitishwa ambayo itakwenda kinyume na maamrisho hayo.” Katiba ndiyo msingi wa nidhamu ya mahakama na kipengee hichi kinaashiria wazi maagizo katika mahusiano baina ya mchakato wa nidhamu ya mahakama ya hivi sasa na Uislamu. Lakini kiukweli badala ya kuagiza nidhamu ya mahakama kuhakikisha kuwa inatumia Quran na Sunnah kama chanzo cha sheria, wameagiza kuwa sheria zitafsifriwe kwa imani ya kisekula.

Hii ni kwa sababu nidhamu ya kisiasa, baraza la mawaziri na taasisi za bunge na mahakama ndani ya nchi za Waislamu zimetokamana na nidhamu za kisekula za utawala wa kikoloni. Ndani ya Pakistan, nidhamu za kisiasa na mahakama zimekitwa juu ya msingi wa Sheria ya Serikali ya India, 1935 ambayo imetokana na utawala wa kikoloni wa Uingereza na ikabakishwa kuwa Katiba shikilizi wakati wa uhuru. Ilhali kumekuwepo na marekebisho katika mitizamo ya katiba, muundo wa mahakama na mchakato kwa kutumia mabaki ya utawala wa Uingereza.

Afghanistan, nayo imeundwa kwa nidhamu ya kisekula. Hata mashirika yasiyokuwa ya Waislamu yanakubaliana na hilo kama ilivyoonyeshwa na ripoti maalum ya USIP (United States Institute for Peace) iliyotolewa mnamo Machi 2015 inayosema kuwa haikowazi ‘migawanyiko’ baina ya mila, sheria za kidesturi na sheria za kidini. Hii ni kwa kuwa nidhamu ya sheria ya nchi inatokamana na machimbuko hayo matatu katika kutafsiri sheria. Katika ripoti hiyo hiyo, shirika hilo linamnukuu kiongozi anayesema kuwa asilimia 99 ya desturi na maadili ya Afghanistan sio ya Kiislamu.

Licha ya hili kuna imani ya kimakosa kwamba dori ya mashirika ya Kiislamu ndani ya nchi hizi huhakikisha kuwa sheria haziendi kinyume na Uislamu, lakini hata wajuzi wa kisheria wenyewe ambao ni wanachama wa mashirika hayo nao pia wanaathiriwa na nidhamu ya kisekula. Kwa mujibu wa muungano wa Wachambuzi wa Afghanistan, wanavyuoni mara nyingi huiunga mkono serikali ili waweze kupata nafasi serikalini. Ndani ya Pakistan, baraza la mfumo wa Kiislamu lina wanachama 8, watatu pekee ni wanachuoni na wanachama wote huchaguliwa na Rais na baraza lake. Hii inaonyesha

***Endelea Uk..9***

wazi kuwa kuna athari ya bunge na baraza la kisekula juu ya mashirika ya Kiislamu. Nidhamu ya kisekula pia imedhibiti nguvu za mashirika hayo mfano Baraza la Mfumo wa Kiislamu na Mahakama za Shariah nchini Pakistan na baraza la Wanachuoni la Afghanistan. Wanaweza kutangaza kuwa sheria fulani sio ya Kiislamu lakini hawawezi kuhakikisha kwamba sheria zenyewe zinabadilishwa. Hii ni kwa mitizamo yote ya hukumu za Shariah ikijumuisha sheria zinazohusiana na wanawake. Mapendekezo ya baraza hilo hayana nguvu. Dori yao ni ndogo na hawana mamlaka ya kuhakikisha kuwa haki za wanawake, zilizodhaminiwa na Uislamu zimepeanwa.

Matatizo yanayohusishwa na hili yanaonekana katika mjadala wa 2016 kuhusiana na sheria dhidi ya dhuluma za kinyumbani ndani ya Pakistan. Ulipigiwa debe na vyombo vya habari, na serikali kama njia ya kuhakikisha kuwa wanaume wanalindwa kutokana na vurugu. Sheria haikupitishwa baada ya Baraza la Mfumo wa Kiislamu kupinga kuwa baadhi ya maelezo yaliyojumuishwa ndani ya sheria hiyo yalikuwa sio ya Kiislamu. Lakini hakuna sheria mbadala iliyowekwa kwa sababu jukumu la Baraza hilo linazunguka katika kutathmini sheria zilizopo na kutoa ushauri kwa serikali ili kufanya mabadiliko. Hivyo basi, matatizo ya wanawake kwa mara nyingine tena hayaku suluhishwa, wala kulindwa chini ya nidhamu ya mahakama na wanawake hawakupata haki dhidi ya walio wakandamiza.

Mahakama iliyoko ina hakikisha kuwa haki za watu fulani zinapatikana lakini watu fulani wanadhulumiwa vibaya mno. Kwa mujibu wa utafiti ambao USIP-PTRO ulifanya na kuegemea katika ripoti maalum ya USIP, baadhi ya migongano baina ya desturi na dini ni juu ya masuala yanayohusiana na ndoa, talaka na haki za mwanamke kurithi.

Katika jamii ya Afghanistan, nidhamu ya mahakama inasemekana inawapendelea wanaume kwa kuwa ina ruhusu kudhulumiwa kwa wanawake. Tafiti ya 2006 iliyofanywa na Haki Duniani (Global Rights), shirika la kimataifa lisilokuwa la kiserikali liligundua kuwa asilimia 85 ya wanawake wa Afghan wameripoti kuwa wamepitia vurugu za kimwili, kingono au kiakili au ndoa za lazima. Ndani ya Pakistan, mfano ni namna haki ya mwanamke kuolewa huondoshwa kwake katika sherehe inayojulikana kama 'Haq bakshish,' ambapo mwanamke huolewa na Quran. Hairuhusiwi katika Uislamu lakini serikali ya Pakistan imefeli kuwalinda maelfu ya wanawake ambao wanalazimishwa kuingia katika hali hiyo. Inacholifanya zoezi hilo kuchukiza zaidi ni kwamba linafanywa ili mali ya familia isitoke nje ya familia.

Tatizo jengine ambalo linajulikana na linawakabili wanawake Pakistan na Afghanistan ni kuhusiana na suala la haki za kurithi. Tafiti iliyofanywa na Pakistan Today, takribani asilimia 60 ya wanawake ndani ya Pakistan hawapati haki yao ya kurithi. Wengine asilimia 40 wanapata lakini hawapewi udhibiti au mamlaka juu ya mali. Lawama juu ya matatizo haya imesukumwa juu ya desturi ndani ya jamii na uzembe wa nidhamu ya mahakama. Ndani ya Afghanistan, wanawake hawajaribu hata kudai sehemu yao ya urithi ili kuhakikisha kwamba wanasimamiwa na familia zao. Haya ni **natija ya desturi na tamaduni zisizokuwa za Kiislamu ambazo zimekitwa ndani ya jamii ya Afghan, na tatizo linaloathiri takribani asilimia 50 ya wanawake wa Afghan.**

Kwa kuhitimisha, nidhamu za mahakama ndani ya ardhi za Waislamu zinakosa uwezo wa kutatua malalamishi kwa njia ya haraka na ukamilifu, zikifeli kutatua matatizo yanayokumba wanawake na familia. Hivyo basi wanaruhusu matatizo kuzidi na kuwa mabaya ikipelekea migawanyiko mikubwa katika ndoa na maisha ya familia. Kujaa, uzembe, gharama kubwa na ufisadi katika mahakama zimekuwa ni vigezo vya kuwakatisha tamaa wanawake wengi katika kupata haki. Suluhisho kwa matatizo ya wanawake sio kuweka viraka vya kibinafsi katika sheria bali ni kuleta mabadiliko msingi kwa jamii yenyewe. Mabadiliko yatakayo osha uchafu wote na kuleta mwamko mpya kupitia utelezwaji wa nidhamu inayo heshimu na kuwalinda wanawake, wanaume, watoto, ndoa na muundo wote wa familia na misingi yake, sheria zake na taasisi za dola. Ni nidhamu ya Kiislamu PEKEE inayoweza kufanya hili.

**Fatima Musab**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 19: Vikwazo Katika Utafutaji wa Nusra Haimaanishi ni Ukoseaji wa Njia/Twariqa



Hakika kukariri kwa utafutaji wa Nusra na kukataliwa na kufeli kila mara, haimaanishi ni ukoseaji wa Twarika au Manhaj, bali inamaanisha kuthubutu katika Twarika/Njia ya kisheria ambayo ametuamrisha Mwenyezi Mungu mpaka kufa.

Mtume (saw) alijitambulisha kwa makabila yafuatayo:

1. Bani Kinda.
2. Bani Kalb.
3. Bani Hanifa.
4. Bani Salamah.
5. Bani Hamadhan.
6. Bani Absi.
7. Bani Ghassan.
8. Bani Fazaara.
9. Bani Murra.
10. Bani Shaiban.
11. Bani Sulaym.
12. Bani Thaa'labah.
13. Ahlu Thaqif.
14. Bani Udhra.
15. Bani Nadhri bin Hawaazin
16. Bani Bakri bin Waail.
17. Bani Amr bin Awf.
18. Bani Al-Haarith bin Kaa'b
19. Bani Aamir bin Swa' swa'h.
20. Bani Qays bin Hutwaym.
21. Kabila mbili za Aws na Khazraji.

Na alikuwa Mtume (saw) anaposikia kuna mgeni amekuja Makkah katika Waarabu, mtu mwenye cheo na Jina, humfuata na kumlingania kwa Mwenyezi Mungu, akamueleza alicho nacho na kumhabarisha kuwa yeye ni Nabii aliyetumilizwa, na alikuwa akiwaomba wamsadikishe na wamhami ili aweze kufikisha risala ya Mola wake.

Na baada ya kutimia Maandalizi ya anga la Madina ili kuipokea dini ya haki, Dini ya Uislamu, kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na kwa kupitia juhudi za balozi wa kwanza Mus'ab bin Umair (ra). Mwenyezi Mungu alimuamrisha Mtume wake (saw) afanye hijra ambayo ni kwa kusimama Dola ya Kiislamu baada ya juhudi kubwa, na damu tukufu zilizo mwagika katika Njia ya Mwenyezi Mungu.

# SWALI/JAWABU:
# Je, "Hesabu" Imeanza Kumaliza Utawala wa Dola Juu ya Uchumi wa Kiulimwengu?



**Swali**

Majaribio yameibuka katika baadhi ya nchi, hususan Urusi, China na Muungano wa Ulaya, ili kubadilisha dola kwa sarafu nyengineyo katika miamala ya kimataifa. Makubaliano hata pia yamefanywa ili kukabiliana na sarafu za nyumbani za baadhi ya nchi, kama vile makubaliano ya Urusi pamoja na India mnamo 31/10/2018, ya kuuza makombora aina ya S-400 kwa sarafu ya Urusi. Na makubaliano yake na Uturuki mwezi mmoja uliopita ya kutumia sarafu za nchi mbili hizi katika biashara ya makombora sawa na hii. Katika mkutano wa Erdogan wa nchi zinazo zungumza lugha ya Kituruki…

China imetangaza kuwa italipia uagizaji wake wa bidhaa za mafuta ya Iran kwa "petro-yuan" na Benki Kuu ya China ilitia saini makubaliano kati ya pande mbili ili kubadilishana sarafu ya nyumbani pamoja na ya mwenzake nchini Japan, bilioni 200 za yuan ($29 bilioni) kwa badali ya yen trilioni 3.4 ($31 bilioni). Je "hesabu" ishaanza kumaliza utawala wa dola juu ya uchumi wa kiulimwengu?

**Jibu**

Ili jibu hili liwe wazi, uhalisia wa msimamo wa dola katika uchumi wa kiulimwengu ni lazima ufafanuliwe:

Kwanza, hadhi ya dola ilianza kuibuka kupitia Makubaliano ya Bretton Woods mnamo 1944, pindi Amerika ilipo lazimisha dola na utawala wake katika mkutano huo, kwa sababu ilikuwa ndio mada iliyokuwa haikuathiriwa katika vita vya dunia … Hivyo basi mfumo wa fedha uliidhinishwa ambapo nchi kuu kumi zilizo endelea kiviwanda zilikubaliana kuweka bei maalumu kwa sarafu zao za nyumbani kwa msingi wa dola ya Kiamerika. Zaidi ya hayo, Amerika ilikubali kuiunganisha dola ya Kiamerika kwa msingi wa dhahabu ($35 kwa kila pauni) na kisha ubadilishanaji wa dola zilizo peanwa na benki kuu kwa bei makhsusi ya dola iliyo unganishwa kwa dhahabu. Hifadhi ya dhahabu nchini Amerika wakati huo ilikadiriwa kuwa thuluthi mbili, na ile ya ulimwengu uliosalia ilikuwa thuluthi moja … lakini kuendelea kudhoofika kwa mizani ya kibiashara ya Amerika kutokana na athari ya matumizi ya nje yalipelekea kudhoofika kwa hifadhi ya dhahabu. Kati ya 1961 na

*Endelea Uk..12*

1970, ilishuka hadi karibu dola bilioni 5. Ili kuhifadhi hazina ya dhahabu ya Amerika, Raisi Nixon aliamua mnamo 1971 kusitisha ubadilishaji wa dola kwa dhahabu, akitangaza mwisho wa mfumo huo uliounganisha dola kwa dhahabu.

Utawala wa Nixon kisha ukakabiliana na mabadiliko haya ya kifedha kupitia msururu wa makubaliano na Saudi Arabia mnamo 1972 hadi 1974, na kuanzisha ile inayoitwa "petro-dola", ukizipa nchi za kigeni sababu nyengine ya kuzikinaisha ya ukusanyaji na utumizi wa dola kwa sababu ya haja yao ya mafuta ambayo yametiwa thamani kwa dola kwa mujibu wa makubaliano na Saudi Arabia, mzalishaji mkubwa zaidi wa mafuta duniani. Saudi Arabia pia ilikubali kurudisha upya mzunguko wa mabilioni ya dola za Kiamerika wa hifadhi ya mafuta kupitia watengezaji zana wa Kiamerika, miundo mbinu na ununuzi wa bondi za Hazina ya Amerika. Kufikia 1977, kwa uchache asilimia 20 ya bondi zote za Hazina ya Kiamerika ng'ambo zilikuwa mikononi mwa Saudi Arabia … endapo mafuta yataongezwa juu ya dhahabu, ambayo pia yametiwa thamani kwa dola, hivyo basi nchi zilikuwa makini kupata dola. Mgao wa hifadhi ya pesa taslimu za dola katika benki kuu duniani ulikuwa ni takriban asilimia 71 hadi 2000, lakini ukashuka baada ya mwaka huu hadi asilimia 62, vilevile asilimia 40 ya deni la kiulimwengu limetawaliwa kwa dola.

Pili: Leo, dola ya Kiamerika inatawala miamala mingi ya kimataifa. Hii imesababisha soko kubwa la kubuni kwa dola ya Kiamerika, linalotafautisha dola ya Kiamerika kutokana na kila sarafu ya kinyumbani ya nchi. Dola imekuwa muamuzi katika miamala iso hesabika yenye thamani ya zaidi ya trilioni 5.4 kwa siku, isiyo husiana na bidhaa au huduma za Kiamerika …

Kinacho shangaza ni kuwa dola inawakilisha asilimia 84.9 ya miamala ya ubadilishanaji wa pesa za kigeni, mbali na miamala ya kibiashara ya Amerika yenyewe kuwa chini ya nusu ya mgao huu, kwa sababu nchi zisizo za Kiamerika huamiliana na dola katika mambo yao ya kibiashara! Nguvu ya kiuchumi ya dola imekusudia kuwa Amerika ina uwezo wa kuliadhibu sio tu taifa lililo lengwa kiuchumi na kifedha; bali pia kuzishajiisha nchi nyenginezo kutokana na kufanya biashara na nchi iliyo lengwa. Amerika ina uwezo wa kufikia hatua hii kali kupitia mfumo wa SWIFT: (Jumuia ya Kiulimwengu ya Mawasiliano ya Kifedha baina ya Mabenki).

Ni nidhamu ya malipo kwa dola. Kwa kuwa dola ndio sarafu ya hazina ya kiulimwengu, SWIFT husahilisha nidhamu ya dola ya kimataifa. Nchi zote ulimwenguni hulipia miamala kupitia kwayo, zikihakikisha kuwa miamala yote kati ya pande mbili imejengwa juu ya dolari. Kwa mfano, Urusi na China haziwezi kubadilishana bidhaa na huduma kupitia pesa zao za nyumbani isipokuwa miamala ya dola ya Kiamerika ilipwe kupitia SWIFT. Amerika yaweza kutumia nihamu hii kulazimisha vikwazo vikali vya kiuchumi. Chini ya nidhamu hii, Amerika ilipiga marufuku, kati ya 2014 na 2015, benki nyingi za Urusi kutokana na SWIFT pindi mahusiano baina ya nchi mbili hizo yalipo zorota. Mnamo Novemba 2018, Amerika ilizindua tena vikwazo vikali dhidi ya Iran kwa kutumia SWIFT. Kampuni nyingi za Ulaya zilikataa kutekeleza biashara zao na Iran kwa kuiogopa Amerika.

Yote haya, kama tulivyo taja awali, ni kwa sababu dola ndio sarafu ya hazina ya kiulimwengu: hisa ya dola katika hazina hiyo ya benki kuu 146 kote ulimwenguni ilifikia asilimia 64 ya hazina zote za sarafu za benki hizo mwishoni mwa mwaka jana. Sarafu ya euro ilichukua nafasi ya pili kwa asilimia 20, huku mchango wa yen ya Japan na pauni ya Uingereza ukiwa ni asilimia 5. Hii ni pasi na kuzungumzia kuhusu yuan ya China, ambayo hazina zake katika benki hizi zilikosa kuzidi dola za Kiamerika bilioni 108, ambayo ni chini ya asilimia 1. (www.alquds.co.uk 19/8/2018)

Tatu: Katika kuangazia hili, nchi za kiulimwengu zilizo na nguvu na umuhimu zilianzisha njia mbili ili kupunguza athari ya dola. Ya kwanza ni msimamo wa Ulaya mnamo 1999, ambapo sarafu ya euro ilitumika rasmi katika biashara, mnamo 2002 katika ushindani na dola. Hii ni kutokana na nguvu ya uchumi wa Ulaya na ujasiri wao katika uwezo wa kushindana. Ya pili ni kupitia nchi, kama Urusi na China, ambazo juhudi zao zilichelewa kuzuia utawala wa dola; hii ni kwa sababu ya kukosa kwao uwezo wa kushindana wakati huo (hadi kuzinduliwa kwa euro) hadi mgogoro wa kifedha wa 2008. Zilihofia kumomonyoka kwa hazina zao za dolari na kupotea kwa thamani yake. Zilijiunga na nchi za kale za Ulaya katika kupunguza utawala wa dola. Kwa kuwa China imekuwa na uchumi mkubwa ulimwenguni, juhudi zake kimataifa zilianza kuathiri utawala wa dola.

Hivyo basi, mgogoro wa kiuchumi wa 2008 ukawa ni mwito wa uamsho kwa nchi ili kufikiria kuhusu dola kama natija ya mgogoro huu. Lakini kilichoifanya hatua hii kuwa ya haraka ni uchokozi wa Trump na vikwazo. Sera mpya iliyo fuatwa na utawala wa Raisi Trump imeharakisha hamu ya dola nyenginezo kuu kuzuia utawala wa dola ya Kiamerika kiulimwengu. Sera ya Raisi Trump ilibeba kwa jeuri mwito wa "Amerika Kwanza", ingawa tawala zote za Amerika kwa yakini zilikuwa zikifanya kazi kwa ajili ya maslahi ya Amerika, lakini utawala wa Trump uko karibu na kutotambua maslahi ya nchi nyenginezo. Trump aliitaka Ulaya kulipia kuanzia nyuma ulinzi wa kijeshi wa Amerika na kuanzisha cheche kali zilizo tishia kuwasha moto wa vita vya kibiashara na China. Alizitaka Japan na Korea Kusini kulipia ulinzi kutokana na makombora ya Korea Kaskazini. Pindi Raisi Trump alipo lazimisha vikwazo juu ya Iran, vilivyomjumuisha kila anayetumia dola kununua mafuta ya Iran, na kwa sababu China kwa sasa ndio muagizaji mkubwa zaidi duniani wa mafuta, vitendo vya Trump viliipelekea China kuchukua hatua kukomesha utumizi wa dola, hususan kwa kuwa imo katika vita vya kibiashara na Amerika. Hivyo basi,

***Endelea Uk..13***

mnamo Machi 2018, soko la hisa la Shanghai lilianzisha mikataba ya wazi ya hisa kwa wawekezaji wa kigeni. Katika mkataba huo, mkataba wa mafuta, ulitawaliwa na sarafu ya yuan ili iwe hasimu kwa Brent na WTI zilizo simama kwa msingi wa dola, ambazo zinatumika kama viwango vya sasa.

Kwa hivyo mgogoro wa kifedha wa 2008, mmuliko wake juu ya uchumi wa nchi nyingi na athari yake kwa mgogoro huu, ikifuatiwa na hisia ya kuhifadhi ya Trump, vita vya kibiashara, na sera za kifedha na kiuchumi … yote yameharakisha miondoko dhidi ya utawala wa dolari.

Nne: Hivyo basi, vitendo hivi vimechochea baadhi ya nchi, hususan zile zenye nguvu za kipekee, na wakati mwengine hata kupita nchi zilizo pambizoni mwa nchi zenye nguvu, ingawa harakati imara na zenye ushawishi ni zile za kutoka kwa dola huru, kwa sababu ushawishi wa dola hizo zilizo izunguka Amerika uko thabiti na kwa lengo maalumu na kisha kusita kwa sababu haziwezi kupinga upinzani imara wa Amerika, maadamu zinazunguka katika duara lake, na tutaregelea vitendo vya nchi hizi:

1- Vitendo vya nchi huru:

A- Urusi: Mnamo 2009, Raisi wa Urusi Medvedev alipendekeza “sarafu mpya ya kiulimwengu” katika kongamano la G8 jijini London kama sarafu badala ili kubadilisha dola. China, Urusi, India, Uturuki na nchi nyenginezo zinazo zalisha mafuta hivi majuzi zilikubaliana “kufanya biashara zao zote na miamala yao yote ya uwekezaji kwa sarafu yao wenyewe.”

Lakini licha ya yote haya, bei ya dhahabu na mafuta ghafi imesalia kuwa kwa dola! Taarifa za kukariri za Urusi za kubadilishwa dola kwa sarafu nyenginezo za kitaifa na kupokea bei ya mafuta ya Urusi kwa sarafu nyenginezo kuliko dola ni kutokana na vikwazo vya Amerika juu ya Urusi baada ya uvamizi wake na kuikalia kwake Crimea na Mashariki mwa Ukraine mnamo 2015. Vile vile ni natija ya uchunguzi juu ya uingiliaji wa Urusi wa uchaguzi wa Amerika wa 2016.

Amerika imeongeza zaidi vikwazo vyake dhidi ya Urusi tangu 2015, na bunge la Congress limepanua zaidi vikwazo, kwa kutumia “Kifungu cha Sheria cha Kupambana na Maadui wa Amerika kupitia vikwazo,” kilichotungwa mnamo Agosti 2017, na kulazimisha vikwazo vikali juu ya Urusi. Hatua hizi zilikuwa kali dhidi ya Urusi, na hili lilikata fungamano la benki kuu nyingi za Urusi na dola, ikipelekea kushuka kwa asilimia 18 ya ruble (sarafu ya Urusi) dhidi ya dola …

Yote haya huku Urusi ikitumia dola katika asilimia 58 ya deni lake, yaani, inakopa karibu nusu ya mikopo yake kwa dola, hivyo Urusi ikaanguka ndani ya matatizo yaliyo isukuma kujaribu kupunguza matumizi yake ya dola, na kujiweka huru kifedha, kiuchumi na kibiashara kutokana na dola.

Putin alisema katika hotuba mbele ya dola ya Duma: “Ni sharti tuimarishe ubwana wetu wa kiuchumi … biashara ya mafuta katika soko la hisa iko kwa dola, na bila shaka tunafikiria namna ya kuuondoa mzigo huu …” aliendelea. “Tumekuwa limbukeni katika miongo iliyopita, tukitaraji kuwa kutakuweko na kujitolea katika misingi iliyotajwa katika biashara ya kiulimwengu na uchumi wa kiulimwengu, na sasa tunaona kuwa sheria za Shirika la Biashara Duniani (WTO) zimekiukwa mno, na kuna vizingiti vimewekwa kwa makadirio ya kisiasa, wanaviita vikwazo” (Duniya Al-Watan, 9/5/2018). Kisha Urusi kidogo kidogo ikapunguza umiliki wake wa bondi za Hazina ya Amerika ambazo zilikuwa zimefikia kileleni mwake mnamo 2008 kwa dola bilioni 223, hadi ilipo kuwa karibu bilioni mia moja mwishoni mwa mwaka jana. Kama natija ya vikwazo vya Amerika juu ya Urusi, Urusi imeachana na nyingi ya bondi zake katika miezi ya Aprili na Mei 2018, na Urusi sasa ina dola bilioni 14.5 za bondi hizo …

Lakini, ruble ya Urusi haiwezi kuchukua nafasi ya dola, kwa sababu ukosefu wa imani katika ruble haiisaidii kuzisukuma nchi zilizo na nguvu kusimama nayo. Hii ni kwa sababu nchi nyingi ulimwenguni hazitaki kununua ruble kwa kuwa ina mwanya mkubwa wa kupanda na kushuka katika masoko ya fedha, na kimsingi ni kwa sababu ulimwengu hauna imani na ruble ya Urusi kama hifadhi ya fedha. Kile ambacho Urusi yaweza kufanya zaidi ni kuzisukuma baadhi ya nchi kulipia ununuzi wa kawi yao ya Urusi kwa ruble, lakini fedha hiyo ya Urusi haiwezi kuchukua nafasi ya dola … msemaji wa Putin Dimitry Peskov alisema katika mahojiano na Runinga ya Rossiya.

“Nchi nyingi zaidi, sio tu upande wa Mashariki lakini pia Ulaya, zinaanza kutafakari njia za kupunguza utegemeaji wao wa dola ya Amerika … Ghafla zimetambua: A. haiwezekani, B. ni lazima ifanywe, na C. jiokoe nafsi yako kama unaweza, yanapaswa kufanyiwa haraka iwezekanavyo.” “Kufutilia mbali dola kwa kiasi fulani kunawezekana, lakini sio kuhusu ima unataka kutoka eneo la dola, bali ni ipi badali kisha: euro? yuan? Au Bitcoin?” “Kila mojawapo ya machaguo haya lina gharama zake, ni sharti tupime gharama za kubakia na dola na gharama za kutafuta msimamo mpya,” alisema Oreshkin, aliyekuwa makamu wa raisi wa Benki Kuu ya Urusi (Financial Times, 3/10/2018). Yote haya yanaashiria kuwa maafisa wa Urusi wenyewe hawajakinai kuwa ruble inatosha kuwa sarafu ya kiulimwengu badala ya dola!

B- China: China inaifanya yuan yake kuwa sarafu mshindani imara wa kiulimwengu, lakini upeo wake wa kisiasa wa kiulimwengu ni mwembamba, hivyo basi kuathiri upeo wake mwembamba wa kiuchumi wa kimataifa katika upande wa ushindani na mzozo

*Endelea Uk..14*

na Amerika. Hivyo basi, haikulazimisha sarafu yake kiulimwengu katika biashara na masoko ya fedha licha ya ukubwa wa uchumi wake, lakini ikatabanni dola, na ikazikusanya kwa viwango vikubwa katika miaka ya hivi karibuni kati ya dola trilioni 3 na 4! Ingawa ilifanya majaribio ya kujiondoa kutoka katika taasisi za kifedha za Amerika, na kuunda jumuia ya kiuchumi BRIX pamoja na Urusi, India, Brazil na kisha Afrika Kusini. Ukubwa jumla wa jumuia ya BRIX ulizidi dola trilioni 15, sawia na asilimia 20 ya uchumi wa kulimwengu wa $ 74 trilioni … pia iliasisi benki ya maendeleo kwa ajili ya kufadhili na kukopesha (jumuia ya BRIC) mnamo Julai 2015 jijini Shanghai ikiwa na mtaji wa dola bilioni 50 hadi hatimaye kufikia dola bilioni 100 kama badala ya Benki ya Dunia, ingawa bado haikuachana na dola!

Pindi Raisi Trump alipo lazimisha vikwazo juu ya Iran na kuvifanya kumjumuisha kila aliyetumia dola kununua mafuta ya Iran, na kwa sababu China kwa sasa ndio muagizaji mkubwa zaidi wa mafuta ulimwenguni, tabia ya Trump ndio iliyoipelekea China kuchukua hatua ili kusitisha utumizi wa dola, hususan kwa kuwa imo katika vita vya kibiashara pamoja na Amerika. Hivyo basi, mnamo Machi 2018, Soko la Hisa la Shanghai lilianzisha mkataba wake wazi wa hisa kwa wawekezaji wa kigeni. Mkataba huu, mkataba wa mbele wa mafuta, ulitawaliwa kwa yuan ili kushindana na mikataba ya Brent na WTI, iliyotawaliwa kwa dola, ambayo inatumika kama viwango vya sasa, hatua zote za juu ziko dhahiri na zaweza kuitingisha dola.

Kinachoidhibiti bidii ya China kuiondoa barabara au kuitingisha dola ni kule kutegemea kwake pakubwa juu ya uchumi wa Amerika na dola. Kiwango cha biashara ya Amerika na China ni kikubwa mno kiko dola bilioni 500 kwa mwaka na sasa ina dola bilioni 1,170 katika bondi za Hazina ya Amerika (tovuti ya gazeti la fedha la China la Xinhua 20/9/2018) chini kutoka dola bilioni 1,300 mnamo 2013, mmiliki mkubwa zaidi wa bondi hizo. Hazina ya dola ya China iko kati ya dola trilioni 3 na 4 zilizo ongezwa katika usafirishaji bidhaa wa China duniani mnamo 2016, zenye thamani ya dola trilioni 2.1 na kuagiza bidhaa za dola trilioni 1.6 kwa mujibu wa Shirika la Biashara Duniani, ikiifanya kuwa nchi ya pili kuu kibiashara duniani baada ya Amerika …

Hivyo basi, uzito wa biashara yao katika dolari, ikiongezewa na bondi za Hazina, inawafanya kuchukua hatua moja mbele na hatua moja nyuma katika kazi makini ya kuitingisha dola. Mafanikio ya Amerika katika kuivutia China kwa biashara ya kimataifa kwa dola imeifanya China kuvutiwa zaidi na kutoitingisha dola. Inajua kuwa itakuwa mwathiriwa mkubwa zaidi duniani wa mtingisho wa dola; hili linaisukuma kupunguza dori yake polepole na kwa uangalifu ili kuhifadhi rasilimali zake za dola na bondi. Na hata kama biashara yote ya China itakuwa kwa Urusi kando na dola, hili halitatui tatizo kwa sababu ukubwa wa biashara ya dola bilioni 120 kwa mwaka katika mielekeo yote miwili (Arabic China 23/9/2018) inabakia kufungika ikilinganishwa na biashara ya kiulimwengu, ambayo ni zaidi ya dola trilioni 20 kwa mwaka. Hivyo, China sio kakamavu kushinda Urusi na ina tahadhari zaidi katika kiu yake ya kuzuia utawala wa dola.

China inaonekana kutambua madhara ya kuamiliana na dola, katika upande wa uzito wa rasilimali zake za dola au katika upande wa bondi za Hazina ya Amerika, nk. Imekuwa nchi inayo nunua dhahabu zaidi duniani, akiba yake ya dhahabu imekuwa kutoka tani 600 mnamo 2008 hadi tani 1,842 mnamo 2018.

Hii inatoa ufafanuzi wa kushuka kukubwa katika hazina yake ya dhahabu, iliyo fikia kilele mnamo 2014 na kuzidi dola trilioni 4 (tovuti ya Trading Economics). Tambua kuwa China imenunua zaidi ya tani 700 za dhahabu mnamo 2015 pekee. Ama kuhusu hazina za Amerika, baada ya mgogoro wa kifedha wa 2008, China ilianza kuziuza. Thamani ya rasilimali zake ilishuka wakati wa miaka miwili baada ya mgogoro huo, lakini tishio la Kiamerika la kuzuia biashara ya China, lililoibuka wakati huo katika kadhia ya usalama wa vikaragosi vilivyo safirishwa kutoka China hadi Amerika, iliifanya kurudi na kupata dola zaidi. Hili liliendelea hadi kufikia kileleni mnamo 2013, lakini China ilirudia kuuza nyuma ya pazia ya vitisho vya kibiashara kutoka kwa utawala wa Trump.

Ilipunguza rasilimali za bondi hizi kwa njia isiyo ya majibizano … na kisha kutafuta njia ya kupunguza dori ya dola katika biashara yake. Ilitia saini makubaliano na Urusi, Japan na nchi nyenginezo kwa ajili ya biashara kwa pesa za kinyumbani. Vile vile iliasisi Soko la Hisa la Shanghai kwa ajili ya biashara ya mafuta iliyo tawaliwa kwa yuan iliyo egemezwa kwa dhahabu, iliyoifanya kushikilia asilimia 10 ya biashara ya mafuta duniani wakati wa miezi sita ya kwanza ya kuasisiwa kwake, ilijiunga na haki maalumu za uchukuaji, (SDR) (yuan inajiunga na dola ya Kiamerika, euro, yen ya Kijapani na pauni ya Uingereza katika kapu la sarafu la SDR, yuan inaongezea kapu la sarafu lililo na haki maalumu za uchukuaji (SDR) moja kwa moja kuanzia 1/10/2016. (https://www.imf.org 30/9/2016)

Lakini, kwa yote haya, uzito wa rasilimali za dola za China, bondi nk. yanaifanya kazi yake ya kuiondoa dola kutokuwa thabiti; hii ndio sababu Yuan inashikilia asilimia 1.7 pekee ya malipo ya kimataifa, ikilinganishwa na asilimia 40 ya dola ya Kiamerika.

C- Muungano wa Ulaya:

Mnamo 1999, euro iliibuka; ilitumika katika mabenki na kubadilisha sarafu za kinyumbani za baadhi ya nchi kama sarafu badala katika Muungano wa Ulaya kuanzia 2002. Ilijaribu kushindana na dola, kwa kuwa nyuma yake zinasimama nchi imara za kiuchumi kama vile Ujerumani na Ufaransa, zikiungwa na nyenginezo zilizo endelea kiviwanda na nchi tajiri. Hivyo basi euro ikawa

***Endelea Uk..15***

ni sarafu yenye nguvu kiulimwengu. Na nyuma yake unasimama mkusanyiko wa nguvu zinazo weza kuwa na athari ya kisiasa ya kiulimwengu inayo shindana na Amerika, na ina uwezo wa kuunda jeshi huru lenye nguvu kama inavyo tafuta. Euro hii imekuwa ndio hazina katika benki kuu za kimataifa kwa asilimia 20-23. Lakini mojawapo ya mambo makuu yanayo zuia euro kutokana na kuutawala uchumi wa kiulimwengu ni udhaifu wa ushawishi wa kisiasa, kijeshi na kiuchumi wa Ulaya kukabiliana na Amerika. Muungano wa Ulaya wenyewe ungali unahami uwepo wake, kwani kuna matishio yanayotishia kwa urahisi uwepo wake, na kujiondoa kwa Uingereza kutokana nao ilikuwa ni mshtuko wa kiujasiri dhidi yake pamoja na kuibuka kwa harakati za kujitenga za ubaguzi wa rangi katika nchi zake, pamoja na matakwa ya kujitenga kutokana na muungano huo, yanayo dhoofisha imani ya Muungano huo … kuongezea ni ukosefu wa umoja katika maamuzi ya kisiasa, yote ni mambo yanayo mulika sarafu ya euro na imani kwake.

2- Dola zinazo zunguka katika duara la Amerika kwa makubaliano ya Urusi, China na Ulaya:

• Uturuki, Iran, India, na Japan:

- Kinara wa Benki Kuu ya Iran Abdul Nasser Hamati alitangaza katika mkutano na wawakilishi wa Urusi na Uturuki kuwa “kadhia ya biashara ilijadiliwa kutumia sarafu ya kinyumbani badala ya dola” (Tehran Times, 9/9/2018)
- Uturuki, Urusi na Iran zimekubaliana kutumia sarafu zao za kinyumbani katika biashara baina yao badala ya dola ya Amerika, shirika la habari la Anatolia liliripoti. Shirika hilo, linalo endeshwa na dola hiyo lilimnukuu gavana wa Benki Kuu ya Iran, Abdul Nasser Hamati akisema jijini Tehran, “miamala ya kibiashara itakuwa ikitumia kiwango maalumu cha ubadilishanaji”. (https://ahvalnews.com/ar 9/9/2018)
- Mnamo Oktoba 2018, China na Japan zilikubaliana kubadilisha dola bilioni 30 ya sarafu, mkataba mkubwa zaidi kufanyika nchini Japan.
“Mkataba wa kusambaza makombora aina ya S-400 kwenda India utafanywa kwa kutumia sarafu ya Urusi ya ruble,” Naibu Waziri Mkuu wa Urusi Yury Borisov alisema mnamo 31/10/2018.

Nchi hizi, ambazo China na Urusi zinajaribu kuleta sera ya kukabiliana na sarafu za kinyumbani, zingali zinazunguka katika duara la Amerika au ni vibaraka wake, yaani, kisiasa zimeunganishwa na Amerika na kwa haraka zimejipanga na Amerika, na hazifanyi maamuzi ya kuachana na kupambana na dola au kuachana na kuifanya kuwa sarafu ya hazina zao za pesa taslim. Uamuzi wa uhuru wa kiuchumi ni lazima ulinganishwe na uhuru wa kisiasa, mithili uhuru wa China na Urusi. Na ikiwa zitakubali kutafiti kupambana na sarafu ya kinyumbani pamoja na Urusi na China, hii ni kwa sababu wamesukumwa na Amerika kutokana na hali ya dharura, lakini pindi itakapomalizika mambo yatarudi kama kawaida:

Tangu vikwazo viwekwe juu ya chuma cha Uturuki, na tangu Amerika iishambulie sarafu ya Uturuki, Erdogan alianza kuikashifu dola kwa ajili ya rai jumla ya nyumbani. Deni jumla la Uturuki la zaidi ya dola bilioni 400 hukusanywa kwa dola, ikimaanisha kuwa kila wakati sarafu yake inashuka thamani dhidi ya dola malipo ya deni yanahitaji lira zaidi na zaidi, na kisha bei kupanda na kuwapa mzigo watu, na Erdogan akitoa hotuba zake za kuzuzua kama kawaida! Taarifa za Erdogan kwa kongamano la sita la Baraza la Uturuki katika Kituo cha Kitamaduni cha Roh Ordu nchini Kyrgyzstan, mnamo tarehe 3 Septemba, ndani yake alisema: “Tunapendekeza kufanya biashara kwa sarafu yetu wenyewe badala ya dola ya Kiamerika.”

Taarifa hii haina uhalisia, na iko mbali na kuwa kweli, kwa sababu Uturuki kimsingi inafanya biashara na EU! Lakini, Uturuki inafanya biashara kwa dola, inakopa kwa dola na nyingi ya hazina zake za sarafu ya kigeni ziko kwa dola, na mafuta, gesi na mali ghafi zinazo agizwa zote ni kwa dola… Tuliiona Uturuki pindi Amerika ilipoondoa vikwazo baada ya mchungaji wa Kiamerika kuachiliwa huru, mambo yalirudi kama kawaida, na ikapoteza ari ya kuupa kipaumbele muamala wa sarafu za nyumbani kabla ya kuondolewa vikwazo … Ama kuhusu nchi zinazo zungumza Kituruki eneo la Asia ya Kati, zinafuata sera ya Urusi, na biashara ya Uturuki kwazo hata kama zinabadilishwa kwa sarafu za kinyumbani hazifikii kiwango cha tarakimu za ushawishi katika biashara ya kiulimwengu kutokana na kutengwa kwa uchumi wa nchi za Asia ya Kati.

Iran imepigwa marufuku kuamiliana na dola kwa sababu ya vikwazo vikali vya kifedha vilivyo ekewa juu yake kwa miaka mingi baada ya kuondolea katika mfumo wa benki wa Kiamerika … Lakini baada ya kuondolewa vikwazo hivyo mnamo 2015, ilikuwa ikiuza mafuta yake kwa dola na kutia saini mikataba mikubwa na kampuni za kimataifa, ikiwemo kampuni za Ulaya kama vile Airbus na Total na kampuni ya Kifaransa kwa dola pekee, kana kwamba hakuna kitu chochote kilichotokea! Vikwazo hivyo na kuondolewa kwake vimeathiri matendo ya Iran kwa muda muwafaka. Amerika ndio inayo iingiza au kuitoa Iran kutoka katika nidhamu ya kibiashara (SWIFT) kwa dola. Amerika inapoongeza taarifa zake dhidi ya Iran na kufunga milango yake ya dola, majibu ya Iran ni taarifa kwamba haitaamiliana na dola.

Ama kuhusu India, tangu jadi inaagiza silaha za Urusi na Amerika haijali hilo. India ina nafasi maalumu kwa Amerika kwa sababu inaitaka iwe nguvu muhimu ya kupambana na ongezeko la ushawishi wa China barani Asia. India inajua hilo, kwa hivyo India haitarajiwi kutafuta mabadiliko ya dola kwa ruble au yuan kama sarafu ya kiulimwengu.

*Endelea Uk..16*

Japan, inayo nasibishwa na Amerika, haihitaji kuelezwa kwa kina. Kuamiliana kwake na Urusi haimaanishi kuwa wako dhidi ya dola au kwamba wanaikubali ruble kama badali ya dola.

Kwa kutamatisha, nchi ambazo zaweza kusemwa kuwa na athari thabiti juu ya kuondolewa kwa dola kutoka katika cheo chake ni Urusi, China na Muungano wa Ulaya. Lakini kila moja ya nchi hizi zina mambo yanayo dhoofisha harakati yao kama tulivyo fafanua, lakini endapo watayaondoa mambo hayo, zinaweza kuiondoa dola kutoka katika cheo chake. Ikiwa hazitafanya kazi juu ya jambo hili, watashtushwa na ile inayoitwa "dola hafifu" na utajiri wao wa hazina ya dola utapotea. Amerika inateseka kutokana na deni kubwa. Kwa mujibu wa Washington Examiner, jarida la Kiamerika, mnamo 1/10/2018, "deni la serikali ya Amerika limekuwa kwa zaidi ya dola trilioni 1.2 wakati wa mwaka wa matumizi ya serikali uliomalizika mnamo 30 Septemba 2018 kwa mujibu wa mtandao wa serikali unaofuatilia deni hilo.

Deni la kitaifa la Amerika mwishoni mwa mwaka wa matumizi ya serikali wa 2017 limefikia 20.25 trilioni …" Mrundiko wa deni la Kiamerika kwa miongo kadhaa limeitia nchi hiyo katika tatizo la kifedha. Kwani mrundiko huu uliongezeka baada ya mgogoro wa 2008, ukiongezeka kutoka dola trilioni 8 hadi dola trilioni 21 leo, tatizo la kifedha la Kiamerika limekuwa baya zaidi, ambapo Bolton ameliita tishio kwa usalama wa kitaifa, na linahitaji suluhisho ya haraka, yaani, karibuni na hivi punde, na wala si mbeleni … Kutokana na uhalisia huu, suluhisho lililobakia kwa Amerika ili kumudu fedha zake ni kuzalisha pesa zaidi (kuchapisha dola). Kuongeza pesa katika idadi inayo kimu ufadhili wa dola, mbali na kulipa madeni yake, ambayo itapelekea kuporomoka kwa dola hiyo, au kile ambacho Waziri wa Hazina wa Amerika alikiita "dola hafifu", akimaanisha kupotea kwa sehemu ya utajiri wa nchi za kiulimwengu zinazo amiliana na dola katika biashara zao, hazina za fedha zao, na bondi za hazina ya Amerika, hasara kama vile kudhoofika kwa dola, ambapo itakuwa ni pigo kwa nchi hizo!

Lakini, uhalisia wa sasa ni kuwa nchi hizi haziwezi kutabanni sarafu ya kiulimwengu badala ya dola lakini, inawezekana kusema kuwa majaribio ya Urusi na China ya kuamiliana na sarafu za kinyumbani na kufanya mikataba na nchi nyenginezo kwa sarafu za kinyumbani, yana athari ya kuvunja utawala wa dola ikiwa yataendelea kuwa imara pasi na ulegevu, harakati ya Ulaya sambamba na China ina athari kubwa. Matakwa ya kununua dhahabu yatatilia nguvu hilo, hayatatui tatizo maadamu itabakia kuwa bidhaa katika benki kuu inayo uzwa kwa dola inapo hitajiwa na dola, au hazina ili kuisaidia sarafu ya karatasi ya dola ili kuiwezesha kufikia sarafu madhubuti. Lakini haitatatua tatizo hilo, mpaka dhahabu na fedha ziwe sarafu na noti za benki zichapishwe na ziwe kwa thamani ya dhahabu au fedha, na sio tu zitumiwe kama bidhaa katika benki za kununulia ile inayo itwa sarafu madhubuti. Hii yamaanisha kuwa Benki Kuu ya kila nchi itatoa sarafu kwa dhahabu na fedha, inakubalika kuchapisha noti za benki kwa thamani ya dhahabu na fedha, na mmiliki wake atakuwa na haki wakati wowote kwenda benki na kuchukua thamani ya dhahabu au fedha badala yake, yaani kuitumia kama sarafu badala ya dhahabu na fedha lakini kwa thamani ya dhahabu na fedha iliyo andikwa katika noti ya benki … kwa hivyo dhahabu na fedha zitatawala. Na kisha hakuna nchi yoyote itakayo weza kufuja utajiri wa wengine au kudhulumu juhudi zao na kupeleka mashini ya vita na kuanzisha vita vyake viovu kwa noti zisizo na thamani kama tuonavyo sasa. Hakuna dola yoyote itakayo weza kufanya hivi, bali dola ya Khilafah, ambayo yaweza kutekeleza hilo kwa sababu ni hukumu ya kisheria iliyo amrishwa na Mwenyezi Mungu, na ilitekelezwa na Mtume wake (saw) katika dola yake, na kufuatiwa na makhalifa waongofu na makhalifa waliowafuata hadi kuvunjwa kwa Khilafah 1342 H sawia na 1924 M, kisha batili ikatawala … Mfumo wa kirasilimali umetawala ulimwengu, wamiliki wake wanachojua ni uporaji na kula pesa za watu kwa batili na ukusanyaji wa pesa kwa mabilioni. Ni dhuluma ya sheria ya binadamu, na tunaona natija haribifu ya migogoro ya kifedha na fadhaiko la kiuchumi ikiongezewa na kuutumia vibaya uwezo wa watu na kupora utajiri wao na kupotea kwa pesa zao kama makaratasi yasiyo na thamani yoyote! Ni muhimu kuangamiza mfumo huu batili na kufanya kazi kwa ajili ya ubwana wa mfumo wa Kiislamu mfumo wa haki na uadilifu uliojifunga ndani ya dola yake ambayo Mwenyezi Mungu amewaahidi waumini wake wenye ikhlasi, wafanyikazi wema:

(وَعْدَ اللَّهِ لَا يُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ)

"[Ni] ahadi ya Allah. Mwenyezi Mungu, hakhalifu ahadi yake, lakini wengi wa watu hawajui" [Ar-Rum: 6]

Ulimwengu utabakia katika matatizo ya kifedha na kiuchumi maadamu hauhukumu kwa sheria ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mkweli

(وَمَنْ أَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكاً)

"Na yeyote anayeupa nyongo utajo wangu – kwa hakika atakuwa na maisha ya dhiki, na Tutamfufua kipofu Siku ya Kiyama." [Ta-Ha: 124]

**18 Rabii' Al-Awwal 1440 H**
**26/11/2018 M**


Email: info@uqab.or.ke